



ISSN 1821-9039 | [www.sematanzania.org](http://www.sematanzania.org) | Issue #18


# Semama

Tanzania's Magazine for Children

*It's possible*



**Zungumza!**  
Timiza wajibu!





# Sema

*It's Possible*

'C' stands for 'Change'. It also stands for 'Children'. And 'SEMA' is Kiswahili for 'SPEAK' ~ We believe that children can bring positive change in their society if they are given a chance to SPEAK & BE HEARD.

We give children different platforms where their voices can be heard. Through the National Child Helpline (116), Happy & Sad Opinion Letters and this magazine, we collect their voices and share them with the world.



@SemaTanzania



Sema Tanzania



Sema Tanzania



UNITED NATIONS  
TANZANIA



Wizara ya Kazi, Uwezeshaji,  
Wazee, Wanawake na Watoto



Save the Children



Segal  
Family Foundation



[www.sematanzania.org](http://www.sematanzania.org)

# A PEEK AT THE INSIDE



## Managing Editor:

Itanisa Mbise

## Consulting Editor:

Kiiya JK.

## Contributors:

Huwaida Yussuf Ally

Elizabeth Joseph

Fatuma Kamramba

Musa Nyanda B.

Madrasat Nouru Nnabiy – Tazari

UNFPA

## Creative & Layout:

Simiyu Kenn

## Cover Illustration:

Emmanuel Mtawa

## Printing:

Jamana Printers

# YALIYOMO

Neno Kutoka Sema	4
Ninawezaje Kujilinda Dhidi ya Udhalilishaji?	5
Shikilia Ndoto Yako	6-7
Simulizi   Mkombozi ni Mwanamke	8-10
Ninawezaje Kuwalinda Marafiki Dhidi ya Udhalilishaji	11
Dunia Yenye Usawa	12-13
Jipime Ufahamu	14-15
Story	16-17
Udhalilishaji: Nimueleze Nani?	18-19
Ngonjera	20
Game	21
Fahamu Haki Zako	22-23
Riddles	24
Vitendawili	25
Upo Salama Mtandaoni?	26-27
When I Grow Up   Nikiwa Mkubwa	28-29
116 Stories   Simulizi za 116	30-31
Sema Wazazi: Zijue Haki Muhimu za Mtoto	32-33
Maswali Toka Tumbatu	34
Tafuta Msaada	35



## WORD FROM **SEMA**

Last time we were keen to “Speak Out, and Take Action” and in the same spirit, in this issue, we celebrate the girl child with the slogan “My Voice, Our Equal Future” – which is this year’s theme for the International Day of the Girl Child. Does this mean we are leaving boys behind? Not at all! Women and girls make up half the global population so their rights are relevant for both boys and girls.

Just like our name suggests, at SEMA we have always believed that the voices of children and young people are key to bringing positive change. What does that mean to you? In what ways are you using your voice to ensure rights of both girls and boys are met? Your voices are key to fighting Violence Against Children and Gender Based Violence and throughout this issue we’ve shown you different ways and places that you can speak out against violence.

In between the serious articles, we’ve put in different games and challenges for you to try with your friends and family. Have fun trying!

We would love to hear your voices. Send in your stories, poems & pictures to SEMA and you could see them in the coming issues.

A big THANK YOU to our readers, schools, madrasas, parents and all the organizations supporting us. Our work would not be possible without you!

Remember that each and every one has the responsibility to speak up against violence; to protect themselves, and to protect others – Zungumza, Timiza Wajibu!

Till next time,

Itanisa.

## NENO KUTOKA **SEMA**

Katika toleo lililopita tulikuwa na kaulimbiu isemayo “Zungumza! Timiza Wajibu”. Safari hii tunaadhimisha na kusheherekea Siku ya Mtoto wa Kike 2020 na kaulimbiu isemayo “Sauti Yangu, Kesho yenye Usawa” – Je! Hii ina maana tunawaacha wavulana nyuma? La Hasha! Asilimia 50 ya idadi ya watu ulimwenguni ni wanawake, kwa hivyo haki zao ni muhimu kwetu sote.

Jina letu linajieleza, SEMA tunaamini kuwa sauti za watoto na vijana ni muhimu katika kuleta mabadiliko chanya. Jiulize – je, unatumia sauti yako kwa namna gani kuhakikisha haki za wasichana na wavulana zinatimizwa? Sauti yako ni muhimu katika kupambana na Ukatili na Udhalilishaji Dhidi ya Watoto na Ukatili wa Kijinsia na katika toleo hili tumekuonesha njia na maeneo tofauti ambayo unaweza kuzungumza dhidi ya udhalilishaji.

Tumekuwekea michezo mbalimbali. Jaribu kila mmoja na marafiki na familia yako.

Tungependa kusikia sauti yako. Tutumie hadithi, mashairi au picha na unaweza kuziona katika matoleo yajayo.

SHUKRANI ZIENDE kwa wasomaji wetu, skuli na madrasa zote, wazazi na mashirika yote yanayotunga mkono katika kazi zetu. Bila nyie, tusingeweza kufika hapa.

Kumbuka kwamba kila mtu ana jukumu la kuzungumza dhidi ya ukatili na udhalilishaji; kujilinda, na kuwalinda wengine - Zungumza, Timiza Wajibu!


Hadi wakati mwingine, Furahia...

Itanisa.







# NINAWEZAJE KUJILINDA DHIDI YA UKATILI NA UDHALILISHAJI?



- \* Tatu malumbano kwa hoja, sio ugomvi, matusi, wala ngumi.
- \* Fahamu njia salama za kupita unapokwenda na kutoka skuli pamoja na maeneo jirani, na utembe na wenzako, usikae njiani mahali popote unapokuwa njiani muda wote.



- \* Ziamini hisia zako – kama unahisi kuna hatari, ondoka haraka, hata kama ni kutoka kwa mtu unayemfahamu.
- \* Mtu akikugusa kwa namna isiyo salama; kataa, ondoka na usikae kimya, mwambie mtu mzima unayemuamini.
- \* Wafahamishe wazazi wako kuhusu mtu yeyote anayekupa zawadi mara kwa mara au anayependa kukaa na wewe muda mwingi mkiwa peke yenu.



- \* Kamwe usitunze siri inayokukosesha amani. Hata kama uliahidi kuto sema au unaogopa; mwambie mtu mzima unayemuamini siku zote.
- \* Usitumie pombe na madawa ya kulevya; jiepuche na maeneo pamoja na watu wanaotumia vitu hivyo.
- \* Epuka Matumizi Mabaya na hatarishi ya Mitandao



# Shikilia ndoto yako

Dear Girl and Boy Child,

My name is Amina. I am a working mum with three children. I work every day so that my children have the best chances in life. I want them to stay healthy, go to school and have opportunities when they grow up.

I also support children and young people – just like you – to be able to make healthy decisions through my work at the United Nations Population Fund (UNFPA). Growing up can be hard. You might feel pressured by your peers to behave in a certain way – or you might think you have to put up with certain behaviour – but you don't. You have the right to grow up in a supportive and safe environment, free from violence and abuse, and make your own decisions. At UNFPA I work to ensure that young people know about their rights so that they can have healthy and respectful relationships – and feel able to seek support from health care and other important services when they need it.

In Zanzibar, UNFPA works with the Police Gender and Children's Desk. This is a safe place that girls and boys can visit if they are frightened about violence or have experienced abuse or violence – nobody should put up with violence and nobody needs to know about your visit. The officers there can connect you with services – such as a Youth-Friendly Service Centre or One Stop Centre – where you access support and information that is right for you, including about puberty and the changes you may notice to your body as you grow from a girl/boy to a woman/man.

UNFPA also works with Sheha's and religious leaders – and through community theatre – to build community



support to end violence and other issues such as child marriage and teenage pregnancy that harm young girls. Through our training we also build young people's skills and knowledge so that they can make healthy decisions and protect themselves.

My dream is that all young girls and boys in Zanzibar grow up safely and achieve their goals. I also want to see young people as leaders, making their voices heard, and looking after the well-being of families and communities, extending a hand to those most in need.

Boys and girls, you are the future of the country. You can be anything you dream – Shikilia Ndoto Yako.

# Shikilia ndoto yako

Mpendwa mtoto wa kike na wa kiume,

Naitwa Amina, ni mama muajiriwa mwenye watoto watatu, kila siku nafanya kazi kwa bidii ili watoto wangu waweze kuishi vizuri, wawe na afya njema na elimu bora itayowawezesha kupata na kuchangamkia fursa za maendeleo watakapokua wakubwa.



Kupitia kazi yangu katika shirika la Umaoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), nasaidia watoto na vijana kama nyinyi ili waweze kufanya maamuzi sahihi juu ya Maisha na afya zao. Safari ya kukua siyo rahisi, wakaiti mwingine unaweza kukumbawa na vishawishi vya makundi rika au kuamaua kuwa na tabia fulani ukidhani inafaa kumbe siyo. Una haki ya kukua katika mazingira bora, wezeshi na salama yasiyo na unyanyasaji wala ukatili, na kufanya maamuzi yako mwenyewe. Katika shirika la kimataifa la UNFPA kazi yangu ni kuhakikisha vijana wote wanazifahamu haki zao ili waweze kuwa na mahusiano mazuri yenye afya na ya kuheshimika, pia waweze kupata huduma nzuri za kiafya pale wanapohitaji.

Upande wa Zanzibar, shirika la kimataifa la UNFPA linafanya kazi kwa kushirikiana na dawati la polisi

la jinsia na watoto. Hii ni sehemu salama kwa wavulana na wasichana kuweza kupata msaada pale wanapopitia unyanyasaji na ukatili wa aina yoyote ile. Hakuna mtu anayeweza kufumbia macho ukatili kwa watoto utakapofika pale. Maafisa wapo pale kuweza kukuunganisha na huduma unayoitaka, kwa mfano kituo cha huduma rafiki kwa vijana nakituo cha mkono kwa mkono. Hapo unaweza kusaidiwa kupata maelezo juu ya haki zako, pia maelezo kuhusu kubarehe Pamoja na mabadiliko ya kimwili unayoweza kubaini unapokua kutoka kuwa mvulana au msichana hadi kuelekea kuwa mwanaume au mwanamke.

UNFPA pia inafanya kazi na masheha na viongozi wa dini, na kupitia Sanaa za maigizo kwa jamii ili kuweza kuisaidia jamii kuacha ukatili na unyanyasaji pia kuachana na masuala mengine yanayoathiri ustawi wa mtoto wa kike kama ndoa za mapema na mimba za umri mdogo. Kupitia mafunzo yetu, tumeweza kuwajenga vijana kuwa na ujuzi na uelewa wa kufanya maamuzi yaliyo sahihi na kujilinda wao wenyewe.

Ndoto yangu ni kuhakikisha wavulana na wasichana wote wa Zanzibar wanakuwa salama na wanaweza kutimiza malengo yao, pia nataka kuona vijana wakiwa viongozi na kuweza kupaza sauti ili kuhakikisha jamii na familia zao zipo katika hali nzuri, na kuweza kuwashika mkono wale wenye uhitaji zaidi.

Wavulana na wasichana, nyinyi ni taifa la kesho, unaweza ukawa chochote unachotaka – Shikilia Ndoto Yako.





# MKOMBOZI NI MWANAMKE



Na Huwaida Yussuf Ally

Katika Kijiji kimoja kilichopo Zanzibar, kulikuwa na bwana mmoja aliyekuwa anaitwa Bakari Mkurange ambae alikuwa anaishi na familia yake ya watu watono. Yeye mwenyewe pamoja na mke wake aliekuwa akiitwa Grace. Walifanikiwa kupata watoto wawili mapacha wa kiume waliokuwa wakiitwa Vuai pamoja na Makame. Pia wakabarikiwa kupata mtoto wa kike aitwae Aisha.

Mzee Bakari Mkurange alikuwa ni mkulima mkubwa wa mazao ya vyakula kama vile mpunga, matunda, mboga mboga n.k. Mzee Bakari na familia yake waliishi maisha ya kawaida siyo ya kimaskini wala ya kitajiri.



Mzee Bakari alikuwa anawapenda sana watoto wake wa kiume kuliko mwanae wa kike. Aliwasomesha kwa hali na mali mpaka wakamaliza elimu ya msingi na kwa bahati nzuri, walifaulu vizuri na kuweza kuendelea na elimu ya sekondari katika shule moja mjini Zanzibar.

Kwa bahati mbaya, Aisha hakuweza kuapata haki yake ya elimu. Alijaribu sana kumshawishi baba yake lakini Mzee Bakari hakukubali. Alimfuata mama yake na kumueleza kuwa na yeye ana haki sawa na kaka zake lakini ilishindikana, kwakuwa baba yake alikwisha toa kauli kuwa mtoto wa kike ni bidhaa mbovu haina faida yoyote bali hasara ndani yake.

Kila Aisha aliposikia maneno yale, yalimumiza upya na machozi ya uchungu kumtoka. Mama alitamani sana kumsaidia binti yake lakini ilishindikana kwani katika nyumba ya Mzee Bakari, mwanamke alikuwa hana kauli mbele ya mwanaume, siku zote mwanamke yuko chini ya mwanaume.

Miaka ilipita na Aisha hakuwa na mbinu nyengine yoyote isipokuwa kukubaliana na maamuzi ya baba yake. Alikuwa akifanya kazi zote za nyumbani kama vile kupika, kusafisha, kufua, kuosha vyombo, kuteka maji, kwenda kutafuta kuni nk. Kazi zote hizo alikuwa akizifanya peke yake bila ya msaada wowote tangu akiwa msichana mdogo sana.

Yuai na Makame walisoma mpaka kidato cha sita wakafaulu vizuri wakenda kusomea sheria katika chuo kikuu cha Dar es Salaam. Mzee Bakari alifarijika sana kuona watoto wake wanaendelea vizuri kimasomo akijua kuwa iko siku watakuja kumsaidia.

Siku moja Mzee Bakari akiwa ameketi nyumbani kwake na kupata burudani kutoka kwenye redio yake, alipata ugeni wa watu watano. Wote walikuwa ni wanaume, tena ni watu wazima. Wageni hao walikaribishwa vizuri na wakasikilizwa shida yao. Walikuwa

ni washenga walikuja kuleta barua ya posa kwa binti Aisha.

Bila kusita na bila ya kuwaza, Mzee Bakari alikubali moja kwa moja na taratibu za harusi zikaanza. Japokuwa Aisha hakupendezwa na maamuzi ya baba yake, alikuwa hana budi kukubali japo shingo upande. Harusi ikapita na binti akaelekea ukweni na kuishi na mumewe.

Ilipita miaka mitano. Aisha aliishi kwa tabu sana katika ndoa yake. Alipata mateso makubwa sana kutoka kwa wifizake na wakwe zake. Kwa bahati mbaya, Aisha hakujaliwa kupata watoto kitu ambacho kilifanya shida na mateso kuongezeka siku hadi siku.

Licha ya kwamba Aisha hakupata fursa ya kusoma, alikuwa akivutiwa sana na biashara alizokuwa akizifanya jirani yake. Jirani alikuwa ni mjasiriamali alikuwa anafuma mikoba, majamvi, makawa ya kufunikia chakula na mashuka ya kulalia. Siku moja, Aisha alimfata jirani yake na kumuomba amfundishe na bila ya kusita yule jirani akamfundisha na mwisho wa siku Aisha akaweza kutengeneza vitu na kuviuza akawa anapata fedha. Cha kusikitisha, hela hiyo akiipata, mume wake anakuja anaichukua na kuitumia hali ya maisha ikawa ndo hiyo kila siku.

Miaka ilisogea wale mapacha wawili Yuai na Makame wakamaliza masomo yao na kupata ajira serikalini. Mwezi mmoja kabla ya kuanza kazi walienda kijijini kwao na kusema wanataka kuoa. Mzee Bakari Mkurange bila ya kusita aliwatafutia watoto wake wanawake wazuri na kuwaozesha.



Baada ya kuoa tu, mambo yalibadilika. Mapacha wale waliwadharau wazazi wao na kuwafanya kama vinyago na mwisho wa siku wakafikia hatua ya kuwaita wachawi. Mzee Bakari alipata maradhiya moyo lakini licha ya Habari hizi kuwafikia mapacha wale, hakuna hata mmoja aliyekwenda kumtembelea.

Aisha kusikia baba yake anaumwa na huku akiwa amechoshwa na mambo aliyokuwa akifanyiwa na mumewe pamoja na wakwe zake, aliamua kudai talaka na kurudi kwao ili kuwasaidia wazazi wake. Aisha alihangaika kumtunza baba yake hadi akapona huku akijiendeleza na biashara zake alizofundishwa na jirani zake.

Siku moja Mzee Bakari alimuita binti yake na kumuomba radhi na Aisha kwa moyo mweupe, alimsamehe baba yake na wakaishi kwa raha bila ya shida yoyote.

## Ujumbe kutoka kwa mwandishi.

Haki ni vitu vyote ambavyo kila mtoto anapaswa kuwa navyo, kufanyiwa au kufanya. Watoto wote wana haki sawa. Mfano wa haki hizo ni kusoma, kupata malezi bora, kupata mahala pazuri na salama pa kuishi kuapata upendo wa hali ya juu kutoka kwa wazazi na jamii kwa ujumla.


Ushauri wangu kwa jamii ni tusipende kubagua Watoto. Watoto wote ni sawa. Unayemuona wewe ndie kumbe sie. Pia haki ni kitu ambacho kila mtoto anastahiki kuipata. Tuache udhalilishaji tutoe haki zote sawa kwa kila mtoto, awe wa kike au wa kiume.





# NINAWEZAJE KUWALINDA MARAFIKI ZANGU DHIDI YA UKATILI NA UDHALILISHAJI?

1. Kuwa rafiki; wasikilize ndugu na rafiki zako na uwafaraji kama wakikuambia kuwa wanafanyiwa ukatili au udhalilishaji. Wasaidie kutoa taarifa kwa watu wazima unaowaamini.
2. Tengeneza orodha ya watu na mashirika unaoweza kuwamba ushauri au kuwapa taarifa na ibandike darasani kwako au katika ubao wa matangazo ili kila mtu aione.
3. Fahamisha wenzako juu ya haki za watoto ukatili au udhalilishaji wa watoto skulini na kwenye jamii yako kupitia maigizo, mashairi, ngonjera, nyimbo, ngoma, qaswida, na njia nyingine mbalimbali.
4. Walinde wadogo zako dhidi ya tabia zisizofaa kwa watu wazima au vijana kwa sababu mara nyingi watoto wadogo hawawezi kuzitambua tabia hizi au hata kujilinda wenyewe.
5. Paza sauti kwa ajili ya marafiki zako na watoto wenye mahitaji maalumu; hawa ni pamoja na watoto wenye ulemavu. Wasaidie kupata haki zao pia!
6. Washauri marafiki na wadogo zako wasipende kutembea peke yao wala kupokea zawadi kutoka kwa watu."



**ZUNGUMZA, TIMIZA WAJIBU!**



**Zungumza!**  
Timiza wajibu!



Wizara ya Kazi, Uwezeshaji,  
Wazee, Wanawake na Watoto





# DUNIA YENYE USAWA

Mwaka 1979 Mkutano Mkuu wa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa ulipitisha Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake. Kwa kifupi, Mkataba huu huitwa CEDAW na unawasaidia wasichana kudai haki zao katika hatua zote za maisha yao: tangu wanapozaliwa hadi wanapozeeka.

Je, haki hizi ni zipi? CEDAW ina ibara 30 lakini tutaangazia ibara 16 za kwanza zinazoainisha haki mbalimbali wanawake walizonazo sawa na wanaume na namna nchi zinavyopaswa kuzilinda haki hizi.


## Ibara

- 1. Maana ya Ubaguzi** Tofautisho au katazo lolote litakalofanywa kwa misingi ya jinsia linalowazuia wanawake na wasichana kufurahia haki zao za kibinadamu katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kituamaduni, kiraia au nyingine yoyote kwa usawa na wanaume, bila kujali kama wameolewa au hawajaolewa.
- 2. Hatua za Kisera** Nchi zitatunga na kutekeleza sheria, kanuni na sera zinazokemea tamaduni na mienendo yenye ubaguzi dhidi ya wanawake na wasichana.
- 3. Usawa** Nchi zitachukua hatua stahiki kuhakikisha maendeleo kamili na uendelezwaji wa wanawake na wasichana ili wanufaike na haki zao za msingi kwa usawa na wanaume.
- 4. Hatua Maalumu za Muda Mfupi** Nchi zinaweza kuchukua hatua maalumu za muda mfupi ili kuwainua na kuwawezesha wanawake na wasichana. Hatua hizi hazina lengo la kuwabagua wavulana na wanaume bali zimekusudiwa kuongeza kasi ya usawa wa wanawake na wasichana.



5. **Mitazamo na Mienendo** Nchi zitafanya jitihada kurekebisha mitazamo ya kiutamaduni na kijamii ili kuondokana na mienendo inayoegemea katika kuona kuwa jinsia moja ni bora kuliko nyingine au katika mgawanyo wa nini kifanywe na wanaume na nini kifanywe na wanawake.
6. **Usafirishaji na Ukahaba** Nchi wanachama zitachukua hatua zote muhimu ikiwemo kutunga sheria zitakazowalinda wanawake dhidi ya usafirishaji haramu, aina zote za unyonyaji na utumiaji wa wanawake katika mambo ya ukahaba.
7. **Maisha ya Kisiasa na Umma** Wanawake wana haki sawa ya kupiga kura, kushika wadhifa wa umma na kushiriki katika shughuli za mashirika yasiyo ya kiserikali.
8. **Ushiriki Katika Ngazi za Kimataifa** Wanawake wanapaswa kuwa na uwezo wa kuwakilisha nchi zao katika ngazi za kimataifa na kufanya kazi na mashirika ya kimataifa kwa usawa na wanaume.
9. **Uraia** Wanawake wana haki sawa na wanaume kupata, kubadilisha au kubakiza uraia wao na ule wa watoto wao.
10. **Haki Sawa Katika Elimu** Wanawake wana haki ya kupata elimu ikiwemo mafunzo ya kiufundi, kuendelea na elimu, michezo na misaada ya kimasomo sawa na wanaume. Mitaala iondoe dhana ya kugawa mambo ya wanawake wanaume katika ngazi zote ijumuishe elimu ya afya ya uzazi.
11. **Ajira** Wanawake wana haki ya kufanya kazi, kupewa fursa za ajira, usawa katika malipo, kuchagua taaluma na ajira wanazopendelea, ruzuku za serikali na hifadhi za kijamii, na usalama wa afya katika kazi zao. Ubaguzi kwa misingi ya ndoa, uja uzito, uzazi na utunzaji wa watoto ni marufuku.
12. **Huduma za Afya na Uzazi wa Mpango.** Wanawake wana haki sawa ya kupata huduma za afya ikiwemo afya ya uzazi, huduma za uzazi wa mpango, huduma wakati wa ujauzito namatunzo baada ya kujifungua.
13. **Haki za Kiuchumi na Kijamii** Wanawake wana haki sawa ya kupata marupurupu ya familia, mikopo ya kifedha na kushiriki katika shughuli za burudani, michezo na nyanja nyingine za kiutamaduni.
14. **Wanawake wa Vijijini** Nchi zitathmini matatizo maalumu yanayowakabili wanawake wa vijijini na nafasi yao katika kufanya familia zao ziweze kujimudu kiuchumi pamoja na kulinda haki zao.
15. **Usawa mbele ya Sheria** Wanawake na wanaume wana haki sawa mbele ya sheria. Hii ni pamoja na haki ya kuingia mikataba na kusimamia mali, na kuchagua makazi na sehemu ya kuishi.
16. **Ndoa na Familia** Wanawake wana haki sawa na wanaume ndani ya ndoa ikiwa pamoja na haki ya kupanga idadi ya watoto watakaozaa, majukumu sawa katika malezi, umiliki wa mali na kufanya kazi.





You probably already know that child marriage is one of the violations against children's rights. Perhaps you are even working to fight against it in your community. But: how much do you know about child marriage in your community and around the world? Take the quiz and then turn the page upside down to see if you got the answers right and learn a little more!

- 1. A child is.**
  - A. Anyone below 18 years
  - B. Anyone below 14 years
- 2. Boys do not undergo child marriage.**
  - A. True
  - B. False
- 3. Child marriage also happens in developed countries**
  - A. True
  - B. False
- 4. Child marriage only occurs in rural areas**
  - A. True
  - B. False
- 5. The law in Tanzania prohibits child marriage.**
  - A. True
  - B. False

Although the Law of the Child Act in Tanzania states that a child is anyone under the age of 18, the Law of Marriage Act allows girls to get married if they have reached 15 years (and boys only once they have reached 18 years). This is known as the minimum age for marriage and hopefully the age will be raised to 18 years for both boys & girls soon.

**5. The answer is False.**

Although child marriage is more common in rural areas, children in urban areas are also sometimes forced into marriage at a young age.

**4. Did you say False? Correct!**

Child marriage takes place all over the world, across continents, cultures and religions – even in wealthy countries like the United States and United Kingdom. But it is much more common in developing countries because one of the main driving factors is poverty.

**3. Believe it or not, this is True!**

Although child marriage often affects girls, boys are sometimes forced to marry at a young age too. When this happens, they often have to drop out of school and take unskilled jobs to support their new family. However, when boys are forced to marry at a young age, it is usually to a child bride while most girls who are forced into child marriage are married off to men that are much older than they are.

**2. The answer is False!**

According to the Law of the Child Act (2009) of Tanzania and the UN Convention on the Rights of the Child (UNCRC), a child is anyone who is under the age of 18.


**1. If you answered (a), you are right!**

## ANSWERS:

### Square Challenge:

How many triangles can you count?

I see..... triangles



Send us this page with your solution and stand a chance to win a Mathematics book of your level

# Jipime Ufahamu!



Unafahamu kwamba ndoa za utotoni ni moja ya ukiukwaji wa haki za watoto. Pengine unashiriki katika kupingana na ndoa za utotoni kwenye jamii yako. Lakini je, una ufahamu kiasi gani juu ya ndoa za utotoni katika jamii yako na duniani? Jibu maswali haya kisha geuza jarida juu chini ili kuona kama umepatia majibu na ujifunze zaidi!

1. **Mtoto ni....**
  - A. Mtu yeyote alie chini ya miaka 18
  - B. Mtu yeyote chini ya miaka 14
2. **Wavulana hawaathiriki na ndoa za utotoni.**
  - A. Kweli
  - B. Si Kweli
3. **Ndoa za utotoni ni tatizo katika nchi zilizoendelea pia**
  - A. Kweli
  - B. Si Kweli
4. **Ndoa za utotoni hutokea vijijini tu.**
  - A. Kweli
  - B. Si Kweli
5. **Sheria nchini Tanzania inakataza ndoa za utotoni**
  - A. Kweli
  - B. Si Kweli

## UNAFAHAMU NINI KUHUSU NDOA ZA UTOTONI?

ndoa kwa wavulana hadi wafikihshe miaka 18).  
inaruhusu wasichana kuolewa wakiwa na miaka 15 (na inakataza  
Ingawa Sheria ya Mtoto nchini Tanzania inasema kwamba  
mtoto ni mtu aliye chini ya umri wa miaka 18, Sheria ya Ndoa

### 5. Jibu ni 'Si Kweli'?

mdogo.  
Ingawa ndoa za utotoni hufanyika zaidi vijijini, wakati na umri  
Ingawa ndoa za utotoni hufanyika zaidi vijijini, wakati na umri

### 4. Umejibu 'Si Kweli'? Umepatia?

ndoa hizi ni umasikini.  
katika nchi zinazoendelea kwa kuwa moja ya sababu kuu za  
na Uingereza. Lakini mara nyingi ndoa za utotoni hufungwa  
dini mbalimbali - hata katika nchi zilizoendelea kama Marekani  
Ndoa za utotoni hufungwa duniani kote, katika tamaduni na

### 3. Amin! ustamini hii ni Kweli?

wanauame ambao wamewazidi sana umri.  
wengi ambao huingia katika ndoa za utotoni huozesha kwa  
hivo, kwa kawaida wavulana wanapopozimishwa kuoa wakiwa  
shule na kujitafuta vibarua ili kujikimu wao na familia zao. Hata  
bado watoto. Mara nyingi hii linapotoke hawalazimu kuacha  
wakati mwiringine wavulana pia wanalazimishwa kuoa wakiwa  
Ingawa wasichana ndio wanaathirika zaidi na ndoa za utotoni,

### 2. Jibu ni 'Si Kweli'?

mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18.  
kwa mjiibu wa Sheria ya Mtoto (2009) ya Tanzania na Mkataba  
wa Umjibu wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto (UNCRC), mtoto ni


### 1. Ikiwa umejibu (a), umepatia?

#### MAJIBU:


#### Chemsha Bongo:

Mchoro huu una pambetatu ngapi?

Ninaona pembe tatu



Tutumie ukurasa huu ukiwa umejaza jibu lako na unaweza kujishindia kitabu cha Hisabati cha darasa lako.



# The Lion & The Mouse

Once upon a time, when Lion was asleep in the jungle, tiny Mouse began running up and down the Lion's back. This soon wakened Lion, who caught the Mouse with his huge paw and opened his big jaws to swallow it.

*"Pardon, O King,"* cried the little Mouse: *"forgive me this time and I shall never forget it. Someday, I too may be able to help you."*

Lion roared with laughter at the idea of Mouse being able to help him, that he let him go.

About a year later, or maybe more, Lion was caught in a hunter's trap and try as he might, despite all his strength, Lion simply could not escape.

Just then the little Mouse happened to pass by, and saw the Lion struggling to get free. He quickly remembered that the Lion had once been kind to him so he ran to help. Soon Mouse had gnawed away the ropes that bound the big Lion.

*"Did I not tell you that I would one day help you?"* said the little Mouse as he quickly hurried away.

**Moral of the Story: *Kindness is never wasted.***



# Simba na Panya

Hapo zamani, Simba akiwa amelala msituni, Panya mdogo alianza kucheza mgongoni mwake akikimbia huku na kule. Michezo ya panya huyo ilimuamsha Simba, akamkamata na kutanua mdomo wake mpana wenye meno makubwa akitaka kumeza

*“Samahani, Ee Mfalme,”* alilia Panya kwa sauti yake ndogo: *“tafadhali nisamehe tu kwa leo na sitakusahau. Hata mimi Siku moja, naweza kukusaidi.”*

Simba aliunguruma kwa kicheko kwa wazo la Panya kuweza kumsaidia, lakini akamwacha aende.

Baada ya mwaka mmoja, au zaidi, Simba alinaswa katika mtego wa wawindaji. Alijaribu kadiri alivyoweza, lakini licha ya nguvu zake zote, Simba hakuweza kujinasua katika mtego ule.

Wakati huo, Panya mdogo alitokea, na kumuona Simba akihangaika kwenye mtego ule. Alikumbuka kuwa Simba aliwahi kumtendea fadhila hivyo alimkimbilia na kumsaidia. Panya alitafuna kamba ambazo zilikuwa zimemfunga Simba na si punde, Simba alikuwa huru.

**Hadithi hii inatufundisha kwamba: Fadhila ni hazina na wema hauozi.**



# Nimueleze nani nikifanyiwa

Ni vizuri kuwaeleza wazazi/walezi wetu kila kitu kinachotusibu lakini wakati mwengine tunashindwa kuwaeleza. Uzuri ni kwamba, wapo watu wengine wanaoweza kukusaidia ikiwa wewe, rafiki au mwanafunzi mwenzako amefanyiwa ukatili au udhalilishaji kama huwezi kumweleza mzazi/mlezi.



**Waalimu:** Waalimu hufanya mambo mengi mbali na kukufundisha. Wana wajibu wa kuwalinda watoto maana wao ndio wazazi wako ukiwa mbali na nyumbani. Zungumza na mwalimu wako ikiwa unahitaji msaada.

**Masheha:** Viongozi hawa wana wajibu wa kuwalinda wanajamii ikiwemo wanawake na watoto, kuwaondoa katika mazingira hatarishi na kuwasaidia kupata watoa huduma kama Maafisa Ustawi wa Jamii au Maafisa Wanawake na Watoto.



**Waratibu wa Wanawake na Watoto:** Hawa ni wanaharaka-ti wakujitolea waliopo katika shehia ambao wana wajibu wa kuwalinda wanawake na watoto, kuwaondoa katika mazingira hatarishi na kuwasaidia kupata msaada kwa watu wengine kama Maafisa Ustawi wa Jamii.

**116:** Huduma ya Simu kwa Mtoto. Hii ni huduma ya bure ya simu iliyopo kwaajili ya watoto na watu wazima kuomba msaada pale ambapo watoto wanapofanyiwa ukatili au haki zao zinapokiukwa. Piga simu 116 bure uweze kuongea na washauri rafiki.



# ukatili na udhalilishaji?



**Maafisa Ustawi wa Jamii na Maafisa Wanawake na Watoto:** Kisheria, maafisa hawa wana wajibu wa kuwalinda watoto hivyo unaweza kuzungumza nao ili upate msaada. Mara nyingi wanapatikana kwenye ofisi za wilaya, hospitalini, makao makuu ya wizara na vituo vya mkono kwa mkono.

**Vituo vya Mkono kwa Mkono:** Hivi ni vituo ambavyo mtoto aliyefanyiwa ukatili au udhalilishaji anaweza kwenda kupata msaada kutoka kwa afisa ustawi wa jamii, polisi, na daktari kwa wakati mmoja. Watoa huduma hawa wote watahirikiana kukusaidia na kukulinda. Zanzibar ina vituo vya mkono kwa mkono 7 katika hospitali mbalimbali. Tembelea ukurasa wa 25 utafute vituo hivi katika ramani.



**Kamati za Shehia za Kupambana na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto:** Kamati hizi zinapatikana katika shehia na baadhi ya wazazi ni wajumbe wa kamati katika shehia zao, ili kuwalinda watoto na wanawake na kuwasaidia wanapopata matatizo.

**Madawati ya Jinsia na Watoto ya Polisi** yapo kwa ajili ya kumsaidia mtu yeyote aliyefanyiwa ukatili au udhalilishaji, bila ubaguzi. Mara nyingi wanawake na watoto ndio wahanga wakubwa wa ukatili na udhalilishaji, hivyo watu wengi hufikiria kwamba madawati haya yanatakiwa kuwasaidia wanawake na watoto tu. Lakini Madawati ya Jinsia na Watoto yanatakiwa kumsaidia mtu yeyote aliyefanyiwa ukatili au udhalilishaji – awe mwanamume au mwanamke; kijana au mzee. Maafisa wa Dawati la Jinsia na Watoto hawavai sare za polisi. Badala yake, wanavaa kama wananchi wengine ili uweze kujisikia huru na usiogope ukiwa unazungumza nao.





# QASWAIDA UDHALILISHAJI - MADRASAT NOURU NNABIY-TAZARI



Udhalili watutia huzuni  
wa Zanzibar aaa  
waumini shime na  
tuacheni

1. kudhalilisha  
kumekemewa  
Sana katika aya  
hukuki

Wanawachanga  
wakizawa  
Hutokezewa ouvu  
mwingi

Wana yatima  
wakilelewa  
Kukataliwa hiyo si  
haki

Hata wajane  
na wenye ndoa  
Hukataliwa na  
wamiliki

Tuna husiwa  
tuache haya  
Wa zanzibaria aaaaa

2. Mtume wetu  
kasimuliwa  
Walivyo kuwa  
kaumu hutwi

Adhabu mabaya  
waliyopewa  
Walobobea na  
ulawiti

Aridhi yao  
inyanyuliwa  
Wakafikiwa na  
umauti

Tuna husiwa  
tuache haya  
Wa zanzibaria  
aaa

3. Nasi jamia  
tunahusiwa  
Tuache haya  
tushiriki

Hivyo faraja  
ni kutubia  
Tupate mema siku  
ya dhiki

Kwani adhabu  
ikitolewa  
Hatutokuwa na  
wakubaki

Tunahusiwa  
tuache haya  
Wa zanzibaria aaa

4. Dua kwa mola  
tunaviombea  
Visiwa vyetu  
Zanzibaria

Tupe salama  
mola Karima  
Tujaalie njema  
Khatima



Help Musa  
find his way  
home before  
it gets dark.



Msaidie Musa  
kufika nyumbani  
kabla jua  
halijazama.



# FAHAMU HAKI ZAKO

“Haki” ni vitu vyote ambavyo kila mtoto anapaswa kuwa navyo, kufanya au kufanyiwa. Watoto wote wana haki sawa na karibia kila nchi imekubaliana na haki hizi.

Haki hizi zote zimeshikamana na zote ni za muhimu. Mara nyingine tunatakiwa kufikiria haki za watoto kwa kuzingatia kipi ni muhimu kwa mtoto kulingana na mazingira husika na kipi ni muhimu kwa maisha na ulinzi bila kuleta madhara. Unapoendelea kukua utakuwa na majukumu zaidi, na uwezo Zaidi wa kufanya maamuzi na kutekeleza haki zako.

Azimio la Umoja wa Mataifa linaorodhesha haki za watoto. Haki hizi zinagusa maeneo yote yanayohusu maisha na ustawi wa mtoto na zipo katika makundi makuu ya haki za mtoto ambayo ni haki ya; Kuishi, Kuendelezwa, Kulindwa na Kushirikishwa.

Je, Azimio la Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki za Watoto linasemaje?

## Ibara 1

Watoto wote walio na umri chini ya miaka 18, wana haki hizi.

## Ibara 2

Watoto wote wana haki hizi, haijalishi ni kina nani, mahali wanapoishi, wazazi wao wanafanya nini, wanazungumza lugha gani, au dini yao ni ipi, ni wa kike au wa kiume, tamaduni zao ni zipi, au wana ulemavu, au ni masikini au tajiri, asiwepo mtoto atakayebaguliwa au kutendewa isivyo.

## Ibara 3

Watu wazima wote wanapaswa kufanya matendo yote kwa kuzingatia ustawi wa mtoto na wanapofanya maamuzi wafikiri jinsi yanavyoweza kumuathiri mtoto.

## Ibara 4

Serikali ina jukumu la kuhakikisha haki za watoto zinalindwa, na inatakiwa kusaidia familia kutekeleza haki zao na kutengeneza mazingira ambayo utakuwa na kufikia malengo yako.

## Ibara 5

Familia yako ina jukumu la kukufundisha na kutekeleza haki zako na kuhakikisha haki zako zinalindwa.

## Ibara 6

Ni haki ya kila mtoto kuishi.

## Ibara 7

Ni haki ya kila mtoto kuwa na jina na ni lazima awe na uraia.

## Ibara 8

Ni haki ya kila mtoto kuwa na utambulisho, na kuwa nakumbukumbu muhimu za taarifa zake.

## Ibara 9

Ni haki ya kila mtoto kuishi na wazazi wake baba/mama, isipokuwa pale ambapo kuishi nao kunahatarisha maslahi yake. Mtoto ana haki ya kuendeleza uhusiano/mawasiliano na wazazi pande zote mbili (baba/mama) kama haishi pamoja nao.

## Ibara 10

Ni haki ya kila mtoto na wazazi kuungana hata kama wanaishi nchi tofauti kwa lengo la kuendeleza uhusiano wa wazazi na mtoto.

## Ibara 11

Ni haki ya kila mtoto kulindwa dhidi ya utekaji.

## Ibara 12

Ni haki ya kila mtoto kujieleza na kutoa maoni yake na maoni hayo lazima yachukuliwe kwa uzito na watu wazima.

## Ibara 13

Ni haki ya kila mtoto kufahamu mambo mapya kujieleza kwa wenzake, kuandika na kuchora labda tu uhuru huo uwe unaathiri haki ya mwenzake.

## Ibara 14

Ni haki ya kila mtoto kupewa uhuru wa kufikiri na kuamua dini yake, akisaidiwa na wazazi kutambua mema na mabaya kwa kuzingatia ustawi wa mtoto.

## Ibara 15

Ni haki ya kila mtoto kuchagua marafiki, kukutana na wenzake na kujiunga na kujenga mahusiano na wenzake bila kuvunja uhuru na haki za wenzake.

## Ibara 16

Ni haki ya kila mtoto kupatiwa usiri.

## Ibara 17

Ni haki ya kila mtoto kupata taarifa kupitia habari kwenye redio, magazeti na vitabu. Ni lazima kuwapa watoto taarifa sahihi zenye kuzingatia maadili, mila na desturi bila kuwaharibu watoto.

## Ibara 18

Ni haki ya kila mtoto kulelewa na wazazi inapowezekana.

## **Ibara 19**

Ni haki ya kila mtoto kupata ulinzi dhidi ya kuumizwa na kufanyiwa ukatili wa kimwili na kiakili.

## **Ibara 20**

Ni haki ya kila mtoto kupata matunzo na ulinzi anapokuwa hawezi kuishi na wazazi.

## **Ibara 21**

Ni haki ya kila mtoto asiye na wazazi kupatiwa matunzo na ulinzi anapokuwa anapatiwa hifadhi na kuendelezwa.

## **Ibara 22**

Ni haki ya kila mtoto ambaye ni mkimbizi (yaani ambaye amelazimishwa kuondoka katika nchi yake) kupewa ulinzi na msaada na haki zake zote zilizoainishwa kwenye azimio hili na haki zote katika azimio hili.

## **Ibara 23**

Ni haki ya kila mtoto mwenye ulemavu kupewa elimu maalum na matunzo bora ili yamsaidie kufikia lengo kuu la kujitegemea na kuishi maisha bora.

## **Ibara 24**

Ni haki ya kila mtoto kupata huduma za afya, maji safi na salama, chakula bora, mazingira salama na taarifa za kufanya awe salama.

## **Ibara 25**

Kwa watoto wanaoishi katika vituo wana haki ya kuangaliwa mara kwa mara na sehemu zao kufanyiwa ukaguzi ili kuhakikisha wapo katika hali bora ya uangalizi.

## **Ibara 26**

Ni haki ya kila mtoto kupata hifadhi na msaada toka serikalini na mashirika yanayo shughulikia ustawi wa jamii.

## **Ibara 27**

Ni haki ya kila mtoto kupewa chakula, mavazi na mahali pazuri pa kuishi na mahitaji yake yote muhimu.

## **Ibara 28**

Ni haki ya kila mtoto kupata elimu bora na kuhimizwa kufikia elimu ya juu kadri awezavyo.

## **Ibara 29**

Taifa lihakikishe kuwa elimu inayotolewa inalenga kumjenga mtoto katika utu na heshima, vipaji na kumuandaa mtoto kuwa huru, mchangamfu, mwenye kudadisi na kutatua mambo.

## **Ibara 30**

Ni haki ya watoto wanaotoka katika jamii ndogo zisizo na sauti, kufurahia tamaduni na mila zao, na kuheshimu na kufurahia dini na lugha zao.

## **Ibara 31**

Ni haki ya kila mtoto kucheza na kupumzika

## **Ibara 32**

Ni haki ya kila mtoto kulindwa dhidi ya kazi ambazo zinahatarisha usalama, afya yake, elimu yake na maendeleo yake kwa ujumla. Kama atafanya kazi, ana haki ya kuwa salama na kulipwa malipo stahiki.

## **Ibara 33**

Ni haki ya kila mtoto kulindwa dhidi ya madawa ya kulevya wala kuhusishwa na uzalishaji pamoja na usafirishaji wa madawa hayo.

## **Ibara 34**

Ni haki ya kila mtoto kuwa huru dhidi ya kutumikishwa kingono/mapenzi.

## **Ibara 35**

Mtu yeyote haruhusiwi kusafirisha, kuteka au kuuza watoto.

## **Ibara 36**

Ni haki ya mtoto kulindwa dhidi ya unyonywaji wa aina yoyote ule.

## **Ibara 37**

Mtu yeyote haruhusiwi kumuadhibu mtoto kikatili na kumletea madhara.

## **Ibara 38**

Ni haki ya kila mtoto kupata ulinzi na kuwa huru na vita. Mtoto yeyote chini ya miaka 15 asishiriki na asilazimishwe kuingia vitani au kuhusishwa kwenye majeshi.

## **Ibara 39**

Ni haki ya kila mtoto kupata msaada na matunzo anapoathiriwa na kuumizwa, kutengwa na kunyanyaswa.

## **Ibara 40**

Ni haki ya kila mtoto kupata msaada na huduma zote za kisheria mbele ya vyombo vya sheria.

## **Ibara 41**

Kama sheria, taratibu na viwango vinavyowekwa au vilivyopo katika nchi ni vya juu kulinganisha na vile vya Azimio la Umoja wa Mataifa, ni bora vitumike hivyo.

## **Ibara 42**

Ni haki ya kila mtoto kufahamu kuhusu haki zake! Na watu wazima wanapaswa kufahamu kuhusu haki hizo na kuwasaidia watoto kuzifahamu.

## **Ibara 43 hadi 54**

Ibara hizi zinaeleza jinsi serikali na mashirika ya kimataifa kama UNICEF yatakavyofanya kazi kuhakikisha watoto wanalindwa pamoja na haki zao.



# RIDDLES

1. What has words, but never speaks?
2. What can travel all around the world without leaving its corner?
3. What can fill a room but takes up no space?
4. Two fathers and two sons are in a car, yet there are only three people in the car. How is this so?

5. I have lakes with no water, mountains with no stone and cities with no buildings. What am I?

- 
- A map  
They are a grandfather,  
father and son.  
Light  
A stamp  
A book  
**Answers**





# VITENDAWILI

1. Ajenga ingawa hana mikono.
2. Hamwogopi mtu yeyote.
3. Inaonekana mara mbili katika dakika moja na mara moja tu katika mwaka.
4. Kila siku hupita njia hiyo hiyo bali arudipo hatumwoni.
5. Poopoo mbili zavuka mto.

- Majibu
1. Ndege
  2. Njaa
  3. Herufi "K"
  4. Jua
  5. Macho

# UPO SALAMA MTANDAONI?

Je, matumizi yako ya intaneti/mtandao yakoje? Jibu maswali yafuatayo kisha jumlisha alama zako zote ili ujue upo kundi gani.

## 1. Je, unadhani ni salama kutumia intaneti/mtandao?

- Ndiyo! Ni salama kabisa kwasababu naweza kuitumia nikiwa nyumbani bila wasiwasi.
- Hapana, intaneti imejaa mambo mengi na watu nisiowafahamu ambao sio salama.
- Sifahamu, lakini huwa napenda kucheza gemu na kujifunza mambo mapya mtandaoni. YouTube ni nzuri pia hasa kwa kutizama muziki!

## 2. Unatumia muda gani kiasi gani mtandaoni?

- Kamwe situmii mtandao iwe simu wala Kompyuta.
- Punde tu nitokapo shuleni, natumia kompyuta au simu ya mzazi wangu kucheza gemu na kutembelea tovuti mbalimbali mtandaoni hadi muda wa kulala.
- Siingii mtandaoni kila siku, huwa natumia mtandao masaa machache tu katika wiki.

## 3. Kina nani huwa unawaomba/kuwakubalia urafiki ama kuwafuata katika Facebook, Instagram na kwenye mitandao mingine ya kijamii?

- Wale tu ninaowafahamu na kuwaamini.
- Yeyote tu, sababu napenda kuwa na marafiki wengi.
- Marafiki wa rafiki zangu, hata kama siwafahamu vizuri.



## 4. Mtu akikutusi au kumtusi rafiki yako mtandaoni.

- Achana nae.
- Mtusi pia.
- Omba msaada kwa mtu mzima unayemuamini.

## 5. Utafanya nini endapo mtu uliyefahamiana nae mtandaoni akikuomba mkutane ana kwa ana?

- Nitamwambia mzazi
- Nitamjulisha rafiki yangu ili anisindikize.
- Nitaenda kukutana na rafiki yangu mpya.

## 6. Je, unajua jinsi ya kuwafungia ama kuwashitaki watu wanaokusumbua kwenye mitandao ya kijamii?

- Ndiyo, najua jinsi ya kuwafungia na kuwashitaki watu wanaonisumbua mtandaoni.
- Sikujua kuwa kuna uwezekano wa kuwafungia na kuwashitaki.
- Nafahamu kuwa kuna namna ya kuwafungia na kuwashitaki, lakini sijui jinsi ya kufanya hivyo. Nitajifunza nikikutana na wasumbufu.

## 7. Je? Utafanya nini endapo mpo nyumbani kwa rafiki yako na wanataka kuingia mtandaoni na kutizama vitu unavyokatazwa kutizama nyumbani kwenu?



- Ngoja nitizame tu kwa leo ili marafiki zangu wasinione mshamba.
- Nitawaambia siruhusiwi kutizama na kuwaeleza sababu na kuwashauri tutizame vitu vingine.
- Huwa natizama nikiwa na marafiki zangu na ndio maana huwa tunaenda maeneo ya mbali na nyumbani kwetu kwasababu wazazi wangu wangekasirika.

### 8. Huwa unazungumza na nani kuhusu mtandao pale unapokuwa huelewi ama unataka kufahamu jambo?

- Rafiki zangu
- Wazazi wangu
- Simshirikishi mtu, huwa najifunza tu mwenyewe.

## Matokeo:

### Alama 0-15:

UNAPENDA sana kutumia intaneti na punde tu ushikapo simu, kompyuta ama kifaa kingine, unaingia mtandaoni haraka iwezekanavyo ili uangalie video, uwasiliane na marafiki zako ama kucheza gemu. Ingekuwa ni maamuzi yako, ungekuwa ukitumia muda wako wote mtandaoni kila siku. Sio siri, mtandao ni kitu kizuri na kuna mambo mengi ya kujifunza na kufurahia, lakini kama shilingi ilivyo na pande mbili, kila kizuri kina ubaya wake. Kumbuka kwamba huwafahamu watu unaozungumza nao

mtandaoni labda tu muwe mlishakuwa marafiki kabla, hivyo yakupasa uwe makini na taarifa zako binafsi usizisambaze mtandaoni na wakati wote mshirikishe mtu mzima juu ya kile unachofanya mtandaoni na watu gani unajihusisha nao. Mwisho kabisa usiache kufanya mambo mengine ikiwemo kusoma, kucheza nje na kazi za nyumbani ili kupumzisha macho na ubongo wako. Kila kitu kwa kiasi, ikiwemo matumizi ya mtandao.

### Alama 16-30

Kwa maoni yako, mtandao sio mzuri hata kidogo, umejaa watu hatarishi na mambo mengi mabaya usiyopaswa kutizama wala kusoma. Hujawahi kuzungumza na wazazi wako juu ya matumizi ya mitandaoni na wala huhitaji kujua. Matumizi ya mtandao ni kupoteza muda wako wa kujisomea na ungependa ufanye vizuri darasani. Ingawa uko sahihi kwamba mtandao unaweza kuwa hatarishi, kwa upande mwingine unaweza kunufaika nao hata kwenye kazi zako za shule. Kuna mengi mazuri kuhusu masomo ya hisabati, sayansi, jiografia na historia, kuna mazoezi na video zinazofundisha masomo haya na mengine mengi kupitia mtandao. Ni vyema kwamba umeshaelewa juu ya hatari inayoweza kutokana na matumizi ya mitandao, hivyo utakuwa mwangalifu unapotumia. Hakikisha unamshirikisha mtu mzima unayemuamini juu ya nini unafanya mtandaoni na wafahamishe haraka endapo kuna jambo linakupa wasiwasi.

### Zaidi ya alama 30.

Una uelewa mzuri kuhusu mtandao, jinsi ya kuutumia na umuhimu wa kutunza taarifa binafsi na unafahamu jinsi mtandao unavyoweza kuelimisha na kuburudisha. Uaelewa kuna hatari katika matumizi ya mtandao na kwamba unapaswa kutoa taarifa haraka kwa wazazi au mtu mzima unayemuamini endapo una wasiwasi. Endelea kujifunza na kufurahia matumizi ya mtandao na familia na marafiki zako na kumbuka kutenga muda wa kucheza nje ya nyumba na si kujifungia muda wote. Kuwa muwazi kwa wazazi, waalimu na marafiki na kumbuka kuomba msaada endapo kuna jambo linakupa wasiwasi mtandaoni.



# When I Grow Up, I want to Be A...

## WORD SEARCH

R T S R P I P L N R Q H Q V A M N T A J  
 I P Z X L S M I **E N G I N E E R** E P P G  
 Z I A M U S D H L Y W Z N X V L C V J Y  
 Z X I V M W C W N O Q F P M H N J L C W  
 Y M B D B A A D O C T Y H T S V O F Q O  
 J C P B E U Y S F J X W A V A N E C J S  
 V U N T R G I P T W D R Q F W B A C E R  
 V P S J K J G E P R E S I D E N T O H T  
 B F W P B H H E X T O K V Z Z Y U A B Z  
 M U S I C I A N N W B N C W W Q U I D D  
 S R P O L I C E F R R O A M G Q V Q Z R  
 X E C T X S S N R I Q I C U A Q D L E D  
 Q H F S L E Z V S T P A A E T F N Y G O  
 T T F A R M E R S E C A R X N D W R Y C  
 G A M P E D I T O R P H A R M A C I S T  
 W Z I T F M N C H E F H R Q L S C R E O  
 H D U L O G X L M S Q M F R A T Z K G R  
 A O D D O B V O F F T Q J U R O Y N L U  
 Q H K Z J R D N Q H O E E G T M P L V Y

Everyone has a dream. What do you wish to be when you are older? There are so many careers to choose from that can be done by both men and women. No matter what your gender is, if you work hard, you can succeed in any job. But have you ever seriously considered what you would like to do when you grow up? The following are just some of the jobs you could do. Find these jobs in the wordsearch as shown.

- |               |               |
|---------------|---------------|
| 1. Teacher    | 10. Tailor    |
| 2. Doctor     | 11. President |
| 3. Chef       | 12. Writer    |
| 4. Pilot      | 13. Athlete   |
| 5. Lawyer     | 14. Editor    |
| 6. Pharmacist | 15. Police    |
| 7. Engineer   | 16. Farmer    |
| 8. Plumber    | 17. Astronaut |
| 9. Presenter  | 18. Musician  |

# Nikiwa Mkubwa Ninataka Niwe...

U N S P B J O O D A T V V M J N B K L M  
 Z C E B D R P O L I S I P W K D K W P K  
 W S V S N B E M D K S M W A E R P G Z Z  
 T F V U R T R X R M W M H N T A I L O R  
 C V D N X M S M E W A C V A W W U N R R  
 O T D W I D X W M J K G K R N B V M U T  
 T G S B D X F A A S I D Z I M D X P B W  
 H W K H B Q C S Z F L W S A W I I I A K  
 H Z X B X G I I G U I L X D A J E S N B  
 D A K T A R I L M H X K U H N C S H I I  
 I Q M G I Q A I T C N P B A A I Y I D D  
 K B F R H Y L S C M K U L I M A T N F N  
 O H A S Q A Q H K N G U I E U G U L H J  
 C H M P W T M A L G N G X G Z F Q D C Q  
 M S A M L Y L J S M W A N D I S H I M K  
 E R S J Z C D I U Z H G G F K O S G T X  
 E E I U V Q A T Q R Y P C D I I L O U M  
 H V A B H R Q G V V Y L E H S A S O M M  
 W Z M W A N A A N G A L W R Y K G V O J  
 B S D S E V V R D B T X O L O O Z F B K

Kila mtu ana ndoto. Je, wewe unatamani uwe nani ukiwa mkubwa? Zipo kazi nyingi sana ambazo zinaweza kufanywa na mwanamke au mwanmume. Hijalishi una jinsi gani, ukifanya jitihada, unaweza kufanikiwa katika kazi yoyote ile. Lakini umeshawahi kutafakari kwa umakini kuwa ungependa kufanya kazi gani utakapokuwa mkubwa? Zifuatazo ni baadhi tu ya kazi unazoweza kufanya. Tafuta kazi hizi katika jedwali kama ilivyooneshwa.

- |                 |                 |
|-----------------|-----------------|
| 1. Mwalimu      | 10. Tailor      |
| 2. Daktari      | 11. Rais        |
| 3. Mpishi       | 12. Mwandishi   |
| 4. Rubani       | 13. Mwanaridha  |
| 5. Wakili       | 14. Mhariri     |
| 6. Mfamasia     | 15. Polisi      |
| 7. Mhandisi     | 16. Mkuilima    |
| 8. Fundi        | 17. Mwananga    |
| 9. Mwasilishaji | 18. Mwanamuziki |

# SIMULIZI ZA 116




## LOCAL LEADER CALLS 116

In May this year, a local leader called 116 to report about one of his citizens who had been neglected by her husband, Baba Adam. Baba Adam had moved away with his second wife and left his family with no assistance. Mama Adam was left behind with three children: Adam who was 8 years old, Zawadi who was 4 years old and Bahati who was just six months old. Mama Adam lived in a difficult situation and planned to sell some of her land so as to move back to her parents but her in-laws not only discriminated her, they prevented her from selling or using her land.

The counsellor and local leader discussed this and agreed that she should go to the police to get help. A few days later, the counsellor talked with the leader and he said he had escorted Mama Adam to the police and they had been a great help. She was now able to rent out her fields and keep all the money. The local leader appreciated the 116 services to the community.

Do you have any questions about child abuse? Do you or any of your friends need to talk about abuse? You can call 116 for free and talk to our friendly counselors. Remember;

-  **116** allows you to report about abuse which has happened to you or to any other child.
-  **116** allows you to talk freely about your daily life and difficulties that you face as a child.
-  **116** guides you in matters that you cannot share with anyone else.
-  **116** helps you to know and to adhere to your responsibilities as a child.





## KIONGOZI APIGA SIMU 116

Mnamo mwezi Mei mwaka huu, kiongozi mmoja alipiga simu namba 116 kutoa taarifa juu ya Mama Adam, raia wake ambaye alikuwa ametelekezwa na mumewe. Baba Adam alipata mke mwingine akahama na kuiacha familia yake bila msaada wowote. Mama Adam aliachwa na watoto watatu: Adam mwenye umri wa miaka 8, Zawadi miaka 4 na Bahati aliyekuwa na miezi sita tu. Mama Adam aliishi katika hali ngumu hivyo alipanga kuuza shamba lake ili arudi kwa wazazi wake lakini wakwe zake pamoja na kumbagua, walimzuia kuuza wala kutumia ardhi yake.

Mshauri wa Huduma ya Simu kwa Mtoto na kiongozi wa eneo hilo walijadili suala hili na wakakubaliana kwamba Mama Adam aende polisi kupata msaada. Baada ya siku chache, mshauri huyo alizungumza na kiongozi huyo. Kiongozi alitoa mrejesho kuwa alimsindikiza Mama Adam polisi kama walivyokubaliana na walipata msaada mkubwa. Hatimae Mama Adam aliweza kukodisha shamba lake na kupata pesa ya kujikimu. Kiongozi wa eneo hilo aliishukuru 116 kwa huduma inayotoa kwa jamii.

Je, una swali loyote kuhusu unyanyasaji wa watoto? Je, wewe au rafiki yako anahitaji kuzungumzia ukatili kwa watoto? Mnaweza kupiga simu 116 bure na kuzungumza na washauri wetu. Kumbuka;

- ☎ **116** inakuwezesha kutoa taarifa kuhusu ukatili ambao umetendewa wewe au mtoto mwingine yeyote.
- ☎ **116** inakupa nafazi kuzungumza kwa uhuru kuhusu maisha yako ya kila siku na matatizo ambayo unakutana nayo kama mtoto.
- ☎ **116** inakupa muongozo juu ya mambo ambayo umeshindwa kumshirikisha mtu mwingine.
- ☎ **116** hukusaidia kujua na kuzingatia majukumu yako kama mtoto.



# SEMA WAZAZI

ZIJUE HAKI MUHIMU ZA MTOTO

HAKI YA KUISHI.  
HAKI YA KUENDELEZWA.  
HAKI YA KULINDWA.  
HAKI YA KUSHIRIKI.  
HAKI YA KUTOBAGULIWA.




Watoto ni sehemu muhimu ya jamii na ndiyo tegemeo la kuendelea kwa taifa lolote, hivyo hawana budi kulelewa vizuri na kuendelezwa. Ili wakue vizuri, watoto wana mahitaji ya msingi ambayo kote Duniani yanatengeneza 'haki' zao. Kimsingi haki za mtoto huwa ni wajibu wa mtu mzima kutimiza mahitaji ya mtoto ili awe mwenye afya, apate elimu na ashiriki katika ujenzi wa nchi yake sasa na hasa atakapokuwa mtu mzima.

**Haki ya Kuishi.** Hii inaanza pale mama anapopata ujauzito. Kukua vizuri kwa mimba kunategemea afya, lishe na mazingira anayoishi mama. Pia kuishi kwa mtoto baada ya kuzaliwa kunategemea upatikanaji wa mahitaji ya msingi, ambayo ni chakula cha kutosha na chenye ubora unaotakiwa, huduma bora za afya na ulinzi toka

kwa wazazi, jamii na Serikali. Vifo vya watoto wadogo hutokana na ukosefu wa moja ya mahitaji tajwa hapo juu.

**Haki ya Kuendelezwa.** Kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania, maendeleo ya mtoto yanahusiana na mtoto kuwa na kiwango kinachokidhi makuzi kimwili, kiakili, kiroho, kimaadili na kijamii. Ili mtoto aweze kukua vizuri anahitaji kutunzwa, kuongozwa na kulelewa katika misingi mizuri. Mathalani, kuendelezwa kwa mtoto kimwili ni kukua kimaumbile na uzito kwa uwiano wa umri. Hali hii inategemea lishe na huduma bora za afya ikiwemo kupatiwa chanjo zote muhimu na upatikanaji wa viinilishe vyote muhimu.







rasmi kuanzia umri wa miaka mitatu hadi anapokuwa mtu mzima. Misingi ya ushiriki wa mtoto huzingatia umri na aina ya masuala anayopaswa kushirikishwa. Watoto wanapaswa kushiriki katika michezo na kutengewa maeneo ya viwanja vya michezo katika mazingira ya mitaani na skuli.

**Haki ya Kutobaguliwa.** Ubaguzi wa mtoto umegawanyika katika makundi mbalimbali, katika yote yapo makundi makuu mawili. Ubaguzi wa kijinsia ambao mtoto wa kike au wa kiume anaweza kubaguliwa na wazazi, walezi au jamii. Upo ubaguzi unaotokana na hali yake ya kimaisha kama vile utajiri au umasikini, ulemavu, ugonjwa, uyatima na jinsi anavyoonekana mbele za watu. Mfano wa kuumiza ni ubaguzi wa kimfumo ambapo hapa kwetu takwimu zinaonyesha kwamba ni asilimia moja tu ya watoto wenye ulemavu wanoandikishwa kujiunga na elimu ya msingi. Hii inaathiriwa na mtazamo wa kijamii dhidi ya watoto hawa kwani wazazi 'huwafungia ndani' kuficha 'aibu' hivyo kuwanyima fursa ya kupata elimu.

Maendeleo ya mtoto yanahitaji jitihada toka kwa mzazi, jamii na Serikali kwa pamoja. Kuendelezwa kwa mtoto hujumuisha kuandikiswa shule ili kupata elimu ya awali na msingi Pamoja na kukuza kipaji chake

**Haki ya Kulindwa.** Inahusu kuzuia vitendo viovu wanavyofanyiwa watoto katika hatua za ukuaji wao, kabla na baada ya kuzaliwa. Mathalani, mtoto anahitaji ulinzi dhidi ya kazi nzito zisizowiana na umri wake, kudhulumiwa mali hasa kwa watoto yatima, kutupwa au kutelekezwa na wazazi na walezi, utoaji mimba wa makusudi, kuonewa nk. Sera ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania pia inasisitiza juu ya ulinzi dhidi ya unyanyasaji wa mtoto ikiwemo kukeketwa, kulazimishwa kuolewa/kuoa katika umri mdogo, na udhalilishaji wa kingono.

**Haki ya Kushiriki.** Ushiriki wa mtoto unapatikana pale mtoto anapopewa nafasi kikamilifu katika kutoa mawazo, kushiriki katika maamuzi ya masuala yanayohusu maendeleo yake, nk. katika hatua mbalimbali za ukuaji wake. Kitaalamu hatua za ushiriki wa mtoto huanza



# MASWALI MAZITO KUTOKA KWA WATOTO WA KISIWA CHA TUMBATU



“Vipi kama baba yako mzazi akikuita chumbani akakwambia, mwanangu leo nitakupatia hela ya shule na nitakuongezea itakuwa nyingi kidogo na baada ya hapo akavua mkanda akakubaka utafanyaje?”



“Vipi ukifanyiwa udhalilishaji na mwalimu na kisha akakwambia ukijaribu kumueleza mtu yeyote nitakuachia radhi, je; radhi hiyo inaweza kukupata?”



“Ikitokea nimefanyiwa udhalilishaji na simu haina pesa, nitaipataje namba 116?”

Kwa kushirikiana na Kijiji cha Watoto SOS – Zanzibar mwaka jana, tulipata bahati ya kuwatembelea watoto katika skuli moja Tumbatu kutoa elimu juu ya kujilinda na kuepuka vitendo vya udhalilishaji katika kipindi cha kusherekea sikukuu ya Maulid. Watoto wa darasa la pili walituuliza maswali magumu yaliyololeta ukimya mkubwa katika chumba cha mafunzo baada ya kutusikiliza kwa makini. Mazungumzo yalikuwa marefu siku hiyo lakini leo tumewawekea maswali matatu ili kama umeshawahi kujiuliza maswali haya, na wewe upate jibu.

Hili likitokea, usisite kumueleza mama. Kama hatokusikiliza basi mueleze mjomba, bibi, babu au mwalimu na hata kupiga simu namba 116 endapo hutasikilizwa kabisa. Hata kama unaogopa kiasi gani ama unampenda baba kiasi gani, kubakwa ni kitendo cha kukuumiza. Ni muhimu kuzungumza ili uweze kujilinda na kuwalinda wadogo zako.

“Shule inatakiwa kuwa sehemu salama na mwalimu ni kama mzazi wa pili kwa mtoto awapo shuleni. Kama mwalimu anakuonea hakuna radhi itayokupata ukimwambia mtu mwingine ili kujilinda. hakikisha unatoa taarifa kwa mwalimu unayemuamini na kwa wazazi pia ili waweze kutatua tatizo mapema kukuepusha na madhara ya udhalilishaji. Hata kama una makosa kama mtoto lazima usikilizwe ili usaidiwe kuelimishwa ulipokosea na kuweka amani baina yako na mwalimu ili kukuepusha kuwa mateka wa adhabu.”

“Namba 116 inapatikana bila malipo, hivyo unahitaji simu yenye chaji tu kuipata namba 116 hautozwi, pesa yoyote.”




Katika ukurasa wa 19, umeona sehemu mbali mbali unapoweza kupata msaada iwapo wewe au rafiki yako amefanyiwa udhalilishaji. Mojawapo ya sehemu muhimu ni Vituo vya Mkono kwa Mkono kwasababu unawakuta watoa huduma wote wanaoweza kukusaidia kwa wakati mmoja; Afisa Ustawi wa Jamii, daktari, na polisi wa Dawati la Jinsia na Watoto.



**DAKTARI**



**AFISA USTAWI WA JAMII**



**AFISA DAWATI LA JINSIA**



Zanzibar ina Vituo 7 vya mkono kwa mkono. Je, unaweza kuonesha vipo katika mikoa ipi katika ramani hii?

**Vituo vya Mkono kwa Mkono Unguja:**

- Hospitali ya Mnazi Mmoja – Mjini Magharibi
- Hospitali ya Makunduchi – Kusini Unguja
- Hospitali ya Kivunge – Kaskazini Unguja

**Vituo vya Mkono kwa Mkono Pemba:**

- Hospitali ya Chake-Chake - Kusini Pemba
- Hospitali ya Abdullah Mzee - Kusini Pemba
- Hospitali ya Michweni - Kaskazini Pemba
- Hospitali ya Wete - Kaskazini Pemba.

# KWANINI UPIGE SIMU NAMBA

116  
CHILDLINE ZANZIBAR



+255 624 100 100

## Kutoa Taarifa juu ya:



Ukatili na  
udhalilishaji  
wa kimwili

Ubakaji/Ulawiti  
au udhalilishaji  
mwengine  
wa kingono



Udhalilishaji  
wa kisaikolojia/  
kihisia

Utelekezwaji  
wa watoto

Vitendo vinavyo  
kiuka haki ya mtoto  
kama vile ndoa  
za utotoni.

Migongano ya  
kifamilia  
ambayo  
humuathiri  
mtoto  
kwa namna  
moja  
au nyingine.

